



Je nisikuelezeni kwa kile ambacho ninakiogopea zaidi kwenu nyinyi kuliko hata masihi dajali? Wakasema: Tueleze ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, akasema: Ni shirki iliyofichikana, anasimama mtu kuswali anapendezesha swala yake kwakuwa anaona kuna mtu anamtazama

Kutoka kwa Abuu Saidi Al Khudriy -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Hadithi Marfu'u: "Je nisikuelezeni kwa kile ambacho ninakiogopea zaidi kwenu nyinyi kuliko hata masihi dajali? Wakasema: Tueleze ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, akasema: Ni shirki iliyofichikana, anasimama mtu kuswali anapendezesha swala yake kwakuwa anaona kuna mtu anamtazama".

[Ni nzuri] [Imepokelewa na Ibnu Maajah]

Walikuwa maswahaba wakikumbushana fitina ya masihi dajali na wakiogopesana juu yake, akawaeleza Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- kuwa kuna jambo la haramu analowaogopea kuliko hata hofu ya fitina ya masihi dajali, nayo ni shirki katika nia na makusudio ambayo haonekani kwa watu, kisha akalifasiri hilo kwa kuyafanya vizuri matendo ambayo hutafutiwa kwayo radhi za Mwenyezi Mungu kwaajili ya kuwaonyesha watu.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3333>

